# Changamoto katika Kutathmini Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza katika Kiswahili kwenye Mitihani ya KCPE na KCSE nchini Kenya

*Mary N. Ndung'u*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Tathmini ya ujuzi wa wanafunzi katika elimu ina nafasi kubwa kwa sababu huwa na malengo kama vile kutafuta thamani au ubora wa madhumuni ya masomo yanayowekwa na mwalimu, mbinu za kufundisha na hata thamani ya maarifa yanayopitishwa kwa wanafunzi. Vipengele vya lugha ambavyo huhitaji kutathminiwa kila wakati kupitia tathmini endelevu au baada ya kipindi fulani cha wakati kupitia tathmini tamati ni stadi za kusikiliza, kuzungumza, kuandika, na kusoma. Ikiwa hizi ndizo aina za tathmini maarufu katika kupima viwango mbalimbali vya maarifa, basi pana haja ya kuchunguza jinsi tathmini hizi hususan tathmini tamati katika mitihani ya KCPE na KCSE nchini Kenya inavyofanikisha kupima ujuzi wa wanafunzi katika stadi za kusikiliza na kuzungumza katika lugha ya Kiswahili. Katika kufanya hivyo, makala haya yanaangazia mbinu zinazotumiwa na changamoto wanazokumbana nazo Baraza la Mitihani la Taifa Nchini Kenya (Kenya National Examination Council, KNEC) katika kuandaa tathmini za stadi za lugha hususan kusikiliza na kuzungumza. Aidha, pana haja ya kutoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo. Mtazamo wa Uchanganuzi Matini (Frey, 1999) unatumiwa kuelekeza uchunguzi katika makala haya.**

**Maneno Muhimu:** Tathmini, tathmini endelevu, tathmini tamati, upimaji, ujuzi, Uchanganuzi Matini

**Utangulizi**

Baraza la Mitihani la Taifa nchini Kenya (The Kenya National Examinations Council - KNEC) ni shirika na liliasisiwa kutokana na Sheria za Bunge likiwa na majukumu ya kutunga, kutahini na kutangaza matokeo ya mitihani ya kitaifa katika shule za msingi, upili na vyuo vya kati (KNEC, 2009). Pamoja na majukumu mengine, baraza hili huwa na jukumu kuu la kutathmini wanafunzi baada ya kipindi fulani cha wakati kupitia tathmini tamati.

Tangu enzi za ukoloni, mfumo wa elimu nchini Kenya umekuwa ukitilia mkazo utoaji wa tathmini tamati kama njia ya kuwaweka watahiniwa katika viwango mbalimbali vya maarifa na hapo baadaye kutuzwa vyeti/astashahada na stashahada.

Tathmini ya aina hii hutolewa baada ya kipindi fulani cha wakati; katika mtihani wa KCPE baada ya miaka minane katika shule za msingi, katika mtihani wa KCSE baada ya miaka minne katika shule za upili, na mitihani anuwai baada ya miaka miwili au mitatu katika vyuo vya kati (Republic of Kenya, 1999). Aina hii ya tathmini huwa na lengo la kuchuja, kuwaweka wanafunzi katika gredi mahususi, kuwapanga na kuwapa vyeti vinavyowapa mwelekeo kuhusu mustakabali wao wa maisha. Tathmini tamati hulenga masomo mengi katika viwango hivi vitatu ikiwemo lugha ya Kiswahili. Katika kutathmini lugha ya Kiswahili, stadi za lugha za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika hutathminiwa katika tathmini tamati. Stadi za kusikiliza na kuzungumza huchukuliwa kuwa ndizo stadi muhimu na za kimsingi ikilinganishwa na stadi za kusoma na kuandika lakini zenye ugumu zaidi kutathmini (Lazaraton, na Riggenbach, 1990). Hata hivyo, mitihani mingi katika tathmini tamati hutahiniwa kupitia maandishi ambayo husomwa kimya na kujibiwa kimaandishi jambo ambalo hupuuza uwezo wa mtahiniwa wa kujieleza kimazungumzo kupitia stadi za kusikiliza na kuzungumza. Katika makala haya nimechunguza changamoto ambazo Baraza la Mitihani la Taifa nchini Kenya hukabiliana nazo katika kutathmini stadi za kusikiliza na kuzungumza na mbinu zinazozingatiwa katika kuhakikisha kuwa stadi hizi zinatahiniwa hata kama ni kwa njia ya kusoma na kuandika.

Makala haya yamerejelea kazi wa watafiti wa awali ambao wamechunguza masuala ya tathmini katika mitihani. Nasibi (2003) katika kitabu alichoandika anazungumza kuhusu njia za ufundishaji na ujifunazji kulingana na mitaala anuwai hususan akilenga nchi ya Kenya. Anapendekeza kuwa tathmini yoyote ile inahitaji kulenga maeneo yafuatayo muhimu: malengo yaliyowekwa, muundo wake ulivyoratibiwa, mchakato wa ufundishaji, mchakato wa utekelezaji wa somo na matokeo yake.

Kafwa et al. (2014) nao wanasema kuwa mfumo wa tathmini tamati nchini Kenya katika mitihani ya kitaifa una udhaifu mkubwa ambao unachukuliwa kama 'usokawaida wakati wa mitihani'. Katika makala yao, walichunguza masuala mawili ambayo yanapambanua maana ya elimu na tathmini kwa kuchanganua utendakazi wake, mpangilio na viwango vya tathmini inavyotumiwa. Utafiti wao ulilenga kuchunguza mikakati badala ambayo huweza kufuatwa na wadau katika kuhakikisha kuwa mfumo wa tathmini ni wa kuaminika. Vilevile, walilenga kutafuta njia mwafaka ambazo huweza kutumiwa kupima umilisi wa kiusomi wa mwanafunzi shuleni.

Aidha Piper na Zuilkowski (2015) wametambua kuwa kuna tafiti chache mno ambazo zimefanywa kuhusu suala la umuhimu wa tathmini katika nchi zinazoendelea hususan Kenya. Wanachuguza suala kuhusu ikiwa uwezo au umilisi wa mwanafunzi wa kusoma unastahii kufanywa kupitia usomaji wa sauti au usomaji kimya. Walitambua kuwa kiwango cha usomaji kwa sauti kinachangia pakubwa kiwamgo cha uelewa wa mwanafunzi kuhusu yaliyomo. Walipendekeza kuwa,

nchini Kenya na kwingineko, umilisi wa wanafunzi katika kusoma utathminiwe kupitia usomaji wa sauti kuliko kupitia usomaji kimya.

Naye Murunga (2016) alichunguza athari za mchakato wa ufundishaji katika upokeaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza katika Kiswahili. Alitambua kuwa mikakati iliyopo na inayotumiwa katika ufundishaji na ujifundishaji ni dhaifu. Hili linachangia kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaoshindwa kupokea/kupata umilisi wa stadi ya kusikiliza katika Kiswahili. Anapendekeza kuwa ikiwa kutakuwa na lengo mahususi la ufundishaji wa stadi ya kusikiliza kabla ya ufundishaji wenyewe, basi stadi hii inaweza kuimarishwa miongoni mwa wanafunzi. Panapokuwa na lengo la kutahini na kutathmini baada ya somo au kipindi kilichowekwa kupitia tathmini endelevu au tathmini tamati, changamoto hii inaweza kukabiliwa.

Kadhalika, katika makala haya, mbinu ya uteuzi wa sampuli kimaksudi imetumiwa kuteua karatasi za mitihani ya KCSE na KCPE kati ya mwaka wa 2013 - 2017. Karatasi hizi za mitihani hii ni kiwakilishi cha tathmini tamati katika mitihani ya kitaifa nchini Kenya katika viwango hivi viwili. Aidha mkabala wa kiuchunguzi wa Uchanganuzi Matini umetumiwa kuchanganua matini teule. Uchanganuzi matini ni njia inayotumiwa na wataalam wa mawasiliano kuelezea na kufasiri sifa za ujumbe/habari zilizoandikwa au kurekodiwa, yaliyomo katika matini, kuchunguza muundo wa matini, pamoja na uamilifu wa habari au ujumbe ulio kwenye matini husika (Frey, Botan & Kreps, 1999). Kati ya mitazamo hii minne ya uchanganuzi matini, karatasi hii inazingatia mtazamo wa uchanganuzi wa yaliyomo (content analysis) ili kuchunguza mikakati inayotumiwa na Baraza la Mitihani nchini Kenya kukabiliana na changamoto za kutathmini stadi za kusikiliza na kuzungumza katika mitihani ya Kiswahili ya KCPE na KCSE.

**Utathmini wa Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza**

Tathmini ni mchakato wa kutambulisha na kukusanya habari kuhusu wanafunzi kwa lengo la kutafuta njia za kukabiliana na changamoto zinazotinga ufundishaji na ujifundishaji. Tathmini hutoa uamuzi kuhusu thamani ya viwango vya ujifunzaji na ujifundishaji na huwa kigezo cha kutolea maamuzi na kufanyia marekebisho endelevu (Rossett, 2001). Tathmini huainishwa katika makundi mawili makuu, tathmini endelevu na tathmini tamati. Tathmini endelevu au tathmini ya 'ndani' ni njia ya kupima uwezo wa mwanafunzi, pamoja na vifaa vya kufanikisha ujifunzaji na ufundishaji wakati masomo yanapoendelea. Huhusu mazoezi baada ya somo, mada, juma, au katikati ya muhula wa kipindi cha usomaji. Aina hii ya tathmini hulenga maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji. Pia hutumiwa kupima ufanisi wa mwalimu katika kutimiza malengo ya somo (Guyot, 1978). Kwa upande mwingine, tathmini tamati ni njia ya kupima kufanikiwa kwa shughuli za ujifunzaji na ufundishaji baada ya kukamilika kwa kipindi/kiwango fulani cha wakati aghalabu muhula, mwaka au kiwango cha elimu kama vile shule ya msingi au shule ya upili. Lengo lake ni matokeo mwishoni mwa kipindi/kiwango hicho. Tathmini tamati aghalabu huwa ni mitihani ya kuandikwa ambayo hujumuisha insha, maswali funge,

maswali wazi, maswali ya majibu ya ndio au la, na maswali ya kujaza mapengo. Lengo la tathmini tamati ni kutoa majibu au itikio kuhusu ujifundishaji na ujifunzaji baada ya kipindi fulani kukamilika ili kufanya maamuzi kuhusu hatua atakayochuka mwanafunzi, atakavyojiendeleza kimasomo au kutuzwa cheti.

Tathmini za stadi za kusikiliza na kuzungumza ni muhimu katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili kwa sababu bila tathmini mchakato wa kupata marifa huwa haujakamilika. Pia ni njia mojawapo ya kuwafanya wanafunzi kujifundisha lugha ya Kiswahili kwa umakinifu zaidi. Nchini Kenya, na labda kwingineko, inafahamika kuwa wanafunzi hujifundisha lugha ili kupata alama za juu katika mitihani lakini sio katika kukuza stadi zao za lugha. Tathmini katika stadi za kusikiliza na kuzungumza ni muhimu pia kama ilivyo stadi za kusoma na kuandika. Walimu wengi hukubaliana kuwa, 'ili kuimarisha na kukuza uwezo wa kusikiliza na kuzungumza, basi pana haja ya kuutathmini uwezo huo' (Hughes, 1989: 44). Mwanafunzi anapofahamu kuwa atahitajika kufanya mtihani wa kusikiliza na kuzungumza na kwamba utendakazi wake kimasomo unategemea stadi hizi, basi itawabidi kuweka bidii katika kukuza stadi hizi za kusikiliza na kuzungumza. Kwa kuwa stadi za kusikiliza na kuzungumza hazishirikishwi katika tathmini za mitihani ya KCPE na KCSE kwa njia ya moja kwa moja, walimu na wanafunzi wana mazoea ya kupuuza mazoezi ya stadi hizi iwe ni katika masomo darasani au katika tathmini endelevu.

Hakika, stadi za kusikiliza na kuzungumza ndizo ngumu sana kutathmini. Kufikia sasa hakuna vigezo au njia mahususi za kutathmini stadi hizi katika mitihani ya KCPE na KCSE. Aidha, idadi kubwa ya wanafunzi wanaofanya mitihani hii ni kubwa na hivyo si rahisi kuitathmini. Pia muda uliotengwa wa kutathmini lugha ya Kiswahili huwa mfupi. Zaidi ya hayo, utuzaji wa alama ni changamoto kuu kwa kuwa tathmini hushirikisha sarufi, utamkaji, mwendelezo kimatamshi, yaliyomo, mpangilio wa mawazo, na msamiati. Lengo la tathmini katika kusikiliza na kuzungumza ni kupima uwezo wa mwanafunzi wa kueleza hoja, kukuza mjadala, na kuwasilisha hoja katika lugha ya Kiswahili huku akishirikisha tajriba yake. Kwa mujibu wa (Brown and Abeywickrama, 2010) tathmini katika kusikiliza na kuzungumza inastahili kupima kwa ukamilifu kile inacholenga kupima kama vile matamshi sahihi, iweze kutegemewa hivi kwamba inatoa matokeo yenye ulinganifu sawa kila wakati inapotolewa.

Tathmini ambayo haiwezi kutegemewa hukosa uhalali (Hughes 1989, 2003). Tathmini iweze kupima kwa ukamilifu kile inacholenga kutathmini kama vile ikiwa ni kukariri shairi fulani, mwanafunzi aweze kukariri shairi hilo kwa mahadhi yanayostahili. Pia tathmini inastahili kuwakilisha hali halisi katika mabadiliko ya lugha, yaani iendane na wakati, ikiwa kuna mitindo mipya ya matumizi ya lugha au kuibuka kwa masuala mageni kama vile sayansi na teknolojia, iweze kutahini mambo hayo. Mwisho, iweze kutoa majibu au itikio kwa mwanafunzi na pia kutoa

mwelekeo kuhusu mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji hivi kwamba kama panahitajika marekebisho fulani au mapendekezo fulani, yaweze kutekelezwa.

Mtihani wa KCPE hutolewa ili kupima matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji katika kiwango cha shule za msingi na hutumiwa kuweka msingi wa utuzaji alama na utoaji wa vyeti baada ya kumaliza masomo ya shule ya msingi. Pia hutumiwa kuchuja watakaoendelea na masomo katika ngazi za juu. Mtihani wa KCSE nao hupima maarifa aliyoyapata mwanafunzi baada ya kipindi cha miaka minne katika shule za upili. Mitihani hii haina uwezo wa kuonyesha maendeleo ya mwanafunzi katika stadi ya kuzungumza na kusikiliza na hata kuonyesha maarifa aliyoyapata kufikia kiwango husika. Hata hivyo, katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, pamekuwa na juhudi za kukuza, kuwekeza na kutathmini nyenzo ambazo zinaweza kutumika katika tathmini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza katika mitihani ya kitaifa ya KCSE na KCPE. Juhudi hizi hata hivyo hupima na kutathmini stadi za kusikiliza na kuandika kupitia njia ya mandishi. Swali linaloibuka ni kama tathmini ya stadi hizi kupitia maandishi inaweza kutoa picha kamili kuhusiana na maarifa aliyoyapata mwanafunzi?

**Yanayopendekezwa Kufundushwa Kulingana na Silabasi na Yalivyotathminiwa katika Mitihani ya KCPE na KCSE (2013-2017)**

Kulingana na silabasi ya Kiswahili, katika shule za msingi (KIE 1992) na shule za upili (KIE 1992) nchini Kenya, kuna mada ambazo zimeteuliwa zifundishwe kulingana na malengo yaliyowekwa. Katika ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza katika somo la Kiswahili, kuna malengo maalum na yaliyomo yaliyopendekezwa kwenye silabasi ya Kiswahili. Silabasi ya Kiswahili huandaliwa na Taasisi ya Utungaji Mitaala nchini Kenya (KICD). Malengo maalum humwezesha mtahini kutunga mitihani inayotoa tathmini ya yaliyosomwa katika kila kiwango cha elimu ya shule za msingi na shule za upili. Wakati Baraza linapotunga mitihani halina budi kuzingatia malengo maalum ya somo pamoja na yaliyomo. Kiambatisho 1 kinaonyesha malengo maalum ya kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza katika shule za msingi na za upili nchini Kenya pamoja na vipengele vya kusikiliza na kuzungumza vinavyopendekezwa kufundishwa kulingana na silabasi. Aidha sehemu hiyo inajumuisha sehemu ambazo zimetahiniwa kati ya mwaka wa 2013 hadi 2017 na maswali yaliyotahiniwa. Maswali ambayo yametahiniwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, kati ya mwaka wa 2013-2017 katika mitihani ya KCSE na KCPE mtawalia, ni ithibati tosha kuwa baraza linajaribu kutathmini stadi za kusikiliza na kuzungumza ila wanafanya hivyo kupitia stadi ya kuandika.

**Yaliyotahiniwa na Yalivyotahiniwa katika Mitihani ya KCPE na KCSE kati ya Mwaka wa 2013-2017**

Sehemu hii inatoa mjadala kuhusu maswali yaliyotahiniwa yakilenga stadi ya kusikiliza na kuzungumza katika mitihani ya KCSE na KCPE kati ya miaka ya 2013-2017.

Katika mtihani wa KCPE, baadhi ya sehemu muhimu za stadi ya kusikiliza na kuzungumza zilizotahiniwa pamoja na maswali yake ni kama vile kitendawili ambapo watahiniwa wanatarajiwa kukitegua, shughuli ambayo katika mazungumzo ya kawaida huhitaji watu wawili au zaidi; mmoja akitega huku mwingine akitegua kwa njia ya mdomo. Swali lingine linahusu kuhesabu idadi ya silabi katika maneno ya Kiswahili. Hili ni swali linalomhitaji mtahiniwa kutamka silabi katika neno hilo ili kuzitenga. Hata hivyo mtahiniwa anatarajiwa kuzihesabu kwa kuzitamka kimyakimya na kisha kuandika idadi yake. Sehemu ya methali iliyotahiniwa inamhitaji mwanafunzi kuchagua methali inayolingana na maelezo yaliyotolewa kwenye viteuliwa. Utahini wa methali katika swali unafanyika kimyakimya shughuli ambayo ingeendelezwa kupitia njia ya mjadala, katika vikundi au kupitia kinasa sauti.

Kadhalika, swali lingine linahusu kutoa maana mbili za homonimia. Kama homonimia hizo zingetolewa kwa njia ya matamshi, matamshi hayo yangesaidia kutofautisha maana mbili au zaidi zinazoibuka. Hata hivyo mtahiniwa anahitajika kutumia ufahamu wake kuhusu maana tofauti za msamiati aliofundishwa darasani. Kunayo pia maswali kuhusu tamathali za usemi ambapo mtahiniwa anatarajiwa kuchagua jibu linalobainisha tamathali husika. Maswali kuhusu aina za sentensi kiuamilifu ambazo hutegemea sifa za kiarudhi kuzibainisha yanaulizwa kupitia maandishi. Kupitia matamshi, mtahiniwa ataweza kutamka au kubainisha sentensi agizi kama inavyohitajika na hivyo kudhihirisha umilisi wake wa kutumia sentensi kadhaa kulingana na utendakazi wake. Maamkizi na maagano yanatahiniwa kwa kumtaka mtahiniwa kuteua ulinganifu sahihi wa maagano au maamikizi hayo. Katika ufundishaji, mwanafunzi anastahili kumuamkua au kumuaga mwenzake kwa kutumia maamkizi au maagano sahihi. Hata hivyo, hilo haliwezekani kupitia tathmini ya aina hii. Mwisho, kunayo maswali kuhusu sauti ghuna na sauti mwambatano. Maswali kama haya huhitaji mtahiniwa kusikiliza utamkaji wa sauti ili kubainisha sauti ghuna na sauti isiyo ghuna. Pia utambulishaji wa sauti mwambatano huhitaji mtahiniwa kusikiliza utamkaji wa sauti kadhaa ili kufanya uteuzi wa sauti inayohitajika. Baadhi ya maswali yaliyotahiniwa katika mtihani huu ni pamoja na:

1. Kitendawili, kikigongwagongwa wanawe hutoka nje, ni:
2. Chagua jibu la kitendawili kifuatacho: Mimi ninakula vyakula vinono lakini sinenepi wala sikui.
3. Neno, **kiliundwa**, lina silabi ngapi?
4. Neno, **mkwajuni**, lina silabi ngapi?
5. Chagua methali ambayo inaafikiana na maelezo yafuatayo: tunapaswa kujishughulisha na mambo ambayo yanaonyesha dalili za mafanikio.
6. Methali, Kamba ya mbali haifungi kuni ni kwa wanaotegemea msaada wa walio mbali, maji ya kifuu bahari ya chungu, ni kwa:

7. Gugu ni nyasi ndefu zinazomea katika sehemu tambarare, gugu pia ni:
8. Sentensi, Jedi ni ninga, imetumia tamathali gani?
9. Kauli zilizopigiwa mstari zimetumia tamathali gani? Tui ni chiriku anameza na kutamka maneno mia moja kwa sekunde.
10. Chagua sentensi inayoonyesha hali ya kuagiza. Meza tembe mbili mara moja.
11. Ni jibu lipi lisilolingana na mengine?

    A. alamsiki – binuru B. shikamoo – marahaba

    C. masalkheri- sabalkheri D. hodi – karibu
12. Ni neno lipi lenye sauti mwambatano? A. mvua, B. liwa, C. kunja, D. wayo
13. Chagua jibu lenye sauti sighuna pekee:

    A. ch, f, s, th B. gh, l, m, t

    C. p, ny, n, d D. dh, k, ng', h

Kuhusu tathmini ya mtihani wa KCSE (2013-2017) wanafunzi wote wanaokamilisha masomo yao katika kidato cha nne nchini Kenya isipokuwa wale wenye mahitaji maalum huukalia mtihani wa Kiswahili ambao hujumuisha stadi nne za kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika. Stadi za kusikiliza na kuzungumza kama nilivyotaja hapo awali hutathminiwa kupitia stadi ya kusoma na kuandika. Katika sehemu ya fasihi simulizi, watahiniwa, kwa mfano wanapewa aina ya hadithi wasome kisha wajibu maswali kutokana na hadithi hiyo. Aina hii ya kuuliza maswali haitofautiani sana na maswali ya ufahamu ambapo mtahiniwa husoma kifungu kisha kujibu maswali kutokana na kifungu hicho. Hadithi katika fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo (Wamitila 2004). Kama swali kuhusu hadithi lingetahiniwa kulingana na sifa za hadithi katika fasihi simulizi, basi watahiniwa wangepewa nafasi ya kuisikiliza hadithi kutoka kwa mtambaji au kutoka kwenye kinasa sauti kisha kujibu maswali kutokana na hadithi hiyo kwa njia ya mdomo. Hali si tofauti katika maswali kuhusu aina za nyimbo katika fasihi simulizi. Watahiniwa wakipewa nafasi ya kuusikiliza wimbo kwanza kisha wajibu maswali yanayofuata, wataweza kushirikisha kwa ukamilifu stadi ya kusikiliza na kuzungumza katika mitihani.

Aidha, kunayo maswali yanayohitaji mtahiniwa kutofautisha matamshi ya vitamkwa tofauti kupitia vitanza ndimi. Badala ya kuvitamka vitanza ndimi au kuvisikiliza vikitamkwa, mtahiniwa anahitajika kueleza maana ya vitanza ndimi, kueleza majukumu yake katika jamii, kisha kueleza jinsi ya kuvihifadhi. Swali kama hili linaweza kutolewa kupitia tathmini endelevu ambapo mwanafunzi anapewa mradi wa kukusanya vitanza ndimi kisha kuvihifadhi kwa njia atakayoiteua mwenyewe. Kwa mfano, kwa kuvirekodi ili visikilizwe na kubainisha ikiwa utamkaji wa sauti tata unabainika wazi, n.k. Baadaye alama zitatuzwa kutegemea kazi ya mtahiniwa na kujumuishwa kwenye alama za tathmini tamati. Watahiniwa pia wanatarajiwa kutofautisha sauti kama vile /ng'/, /gh/, kulingana na

sifa bainifu za kila sauti. Ishara za sauti kama hizi zinatolewa katika maandishi. Ingefaa zaidi kwa mtahiniwa kuzitamka sauti hizi kwa sauti kisha kubainisha sifa za kila mojawapo ili kuzitofautisha. Kwa kufanya hivyo, mtahiniwa atakuwa ametathminiwa katika utamkaji wa sauti husika ili kubainisha sifa zake. Maswali zaidi yanahusu silabi kama kipashio cha utamkaji. Kwa kutamka silabi, mtahiniwa ataweza kueleza maana yake, kwamba silabi ni kipashio cha utamkaji kikubwa kuliko fonimu na kidogo kuliko neno (TUKI, 1990). Kwa kuwa silabi ina kilele kimoja cha utamkaji, mtahiniwa akitamka kwa sauti neno alilopewa ataweza kutenga silabi zinazoliunda. Mifano ya maswali yaliyotahiniwa katika mtihani wa KCSE ni:

1. i. Andika aina ya hadithi hii. (ngano/baada ya kuisoma).

   ii. Fafanua umuhimu wa aina hii ya hadithi.

   iii. Fafanua majukumu manne ya fomyula ya kumalizia katika ngano.
2. Jibu maswali yanayofuata (baada ya kusoma wimbo).

   i. Taja majukumu matano ya nyimbo katika jamii.

   ii. Fafanua mambo anayohitaji mwimbaji kufanikisha uwasilishaji wa utanzu wa nyimbo.
3. i. Andika aina ya sifo hii. (iliyotolewa)

   ii. Bainisha shughuli za kijamii na kiuchumi za jamii inayosawiriwa na utungo huu.

   iii. Fafanua mambo matano ya kufanikisha uwasilishaji wa sifo.
4. i. Eleza maana ya vitanza ndimi.

   ii. Fafanua majukumu ya vitanza ndimi katika jamii.

   iii. Eleza mbinu tatu za kukusanya na kuhifadhi habari kuhusu vitanza ndimi.
5. Andika tofauti kati ya sauti zifuatazo:

   i. /ng'/, /gh/,

   ii. /v/, /f/,

   iii. /r/, /l/,

   iv. /m/, /n/
6. Andika sauti zenye sifa zifuatazo: (mfano: nazali ya kaakaa laini)
7. Andika maneno yenye miundo ifuatayo:

   i. K+K+K+I+K+I,

   ii. K+K+I+K+I,

   iii. I+K+K+I
8. Eleza sifa mbili za sauti /dh/.

9. i. Eleza maana ya sauti mwambatano.

   ii. Andika sauti mwambatano inayotamkiwa kwenye ufizi.
10. Tunga sentensi kutofautisha maana ya **rithi** na **ridhi.**
11. Tunga sentensi kutofautisha maana ya **vito** na **fito.**
12. Nini maana ya silabi?
13. Bainisha silabi katika neno, **wanyweshavyo**.
14. Methali, Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi huambiwa mtu anayezidharau shida za wengine, Mtu asiyetambua kuwa kuna wengine wanaoweza kulimudu jambo kuliko yeye huambiwa methali gani?
15. Andika nahau inayojumuisha ujumbe ufuatao: Kumzuia mtu kupata kitu japo huna haja nacho.

Kutokana na mifano ya maswali kutoka mitihani ya awali ya KCPE na KCSE, inabainika kuwa kuna changamoto katika kutahini vipengele vya kusikiliza na kuzungumza katika mitihani ya KCPE na KCSE kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi wanaofanya mitihani hii. Idadi ya watahiniwa imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Kulingana na Ripoti za Mwaka za Matokeo ya Mitihani ya KNEC (2017) katika KCPE na KCSE, mtihani wa KCPE ulikuwa na watahiniwa 839,759 mwaka wa 2013 na 942,021 mwaka wa 2017. Katika mtihani wa KCSE walikuwa watahiniwa 446,696 katika mwaka wa 2013 na 611,952 katika mwaka wa 2017. Vilevile, muda unaotengewa kutoa tathmini za aina hii hauwezi kutosha kupima uwezo wa mwanafunzi wa kushiriki katika mazoezi ya kusikiliza na kuzungumza kwa lengo la tathmini. Isitoshe, tathmini ya aina hii huwa na gharama ya juu kwa sababu inahitaji kushirikisha vifaa na mbinu anuwai wakiwemo watahini watakaoshirikishwa katika utahini.

**Matokeo ya Utafiti**

Baada ya uchunguzi kuhusu tathmini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza katika mitihani ya KCPE na KCSE, inabainika kuwa Baraza la Mitihani la Taifa nchini Kenya linajitahidi kwa sasa kuhakikisha kuwa tathmini ya vipengele vya stadi za kusikiliza na kuzungumza imeshughulikiwa. Katika mtihani wa KCSE, tathmini inashughulikiwa kupitia maswali kwenye sehemu zifuatazo za mtihani:

i. Fasihi simulizi kupitia maswali kuhusu vipera vyake kama vile ngano, nyimbo, semi, n.k;

ii. Ushairi ambapo badala ya kukariri mashairi, mtahiniwa anahitajika kutoa majibu kuhusiana na ushairi kimuundo, kimaudhui, na kimtindo;

iii. Isimujamii kupitia sajili mbalimbali za lugha ambapo watahiniwa wanahitajika kwa mfano, kutambua sajili mahususi na sifa zake;

iv. Matumizi ya lugha ambapo watahiniwa huhitajika kuelezea sifa za matamshi ya sauti za Kiswahili, kutofautisha sauti hizi kulingana na

sifa zake, na kutaja sauti wanapopewa sifa zake za utamkaji. Pia wanahitajika kutenga silabi kwenye maneno badala ya kuzitamka. Aidha watahiniwa huhitajika kutambua au kuandika sauti au silabi mwambatano katika maneno. Shughuli nyingine katika sehemu hii na inayohusu kusikiliza na kuzungumza ni ile ya kutofautisha vitate kwa kutunga sentensi, kufafanua maana za methali na nahau.

v. Uandishi wa insha ambapo watahiniwa badala ya kutoa ripoti, kujadili, au kutoa hotuba kwa njia ya mdomo wakati wa tathmini, wanahitajika kuandika namna ambavyo wanaweza kuwasilisha tungo kupitia maandishi.

Isitoshe, katika mtihani wa KCPE, Baraza la Mitihani la Taifa nchini Kenya limejitahidi kukumbana na tatizo la kutahini stadi za kusikiliza na kuzungumza kupitia maswali ya kuchagua majibu ya maamkizi yaliyotolewa au kulinganisha maamkizi, maswali ya lugha ya adabu na heshima, yenye sauti ghuna na sighuna, yenye sauti za silabi mwambatano na changamano, yenye kutofautisha maana za maneno yenye sauti tata/vitate, yinayolingana na tamathali ya usemi iliyotumika katika sentensi, ya kitendawili kilichotolewa kwenye swali, yenye methali zenye maana zinazolingana au kutofatiana au maana ya methali iliyotolewa katika swali, yenye maswali kuhusu mashairi ya Kiswahili, na ya kuandika insha za maelezo, mijadala, hotuba, masimulizi, na methali ili kupima utungaji wa sentensi nyepesi na sahihi.

Japo makala haya yametambua kwamba ni vigumu kutathmini stadi za kusikiliza na kuzungumza katika mitihani ya KCPE na KCSE, na kwamba Baraza la Mitihani la Taifa nchini Kenya limeweka njia ya kutathmini stadi hizo kupitia maandishi, mapendekezo yafuatayo yanatolewa:

i. Kutathmini kusikiliza na kuzungumza katika Kiswahili inavyofanywa katika mitihani ya lugha nyingine kama vile Kifaransa na Kijerumani.

ii. Kutathmini kusikiliza na kuzungumza katika Kiswahili kupitia tathmini endelevu kama inavyofanyika katika somo la Kilimo ambapo wanafunzi huanza kukaguliwa miradi ya kilimo kuanzia hatua za mwanzo hadi za mwisho za mavuno kutokana na mradi huo. Alama kutokana na mradi huo hujumuishwa na alama za tathmini tamati.

iii. Nchi pamoja na Baraza la Mitihani nchini Kenya watafute mikakati ya jinsi ya kutahini kusikiliza na kuzungumza kupitia stadi zenye na sio kupitia maandishi. Pia nchi iwekeze kwa kununua vifaa vya kutahini stadi za kusikiliza na kuzungumza kama vile tepurekada, kinasa sauti, santuri, video, n.k.

iv. Kuzingatia au kutilia maanani mapendekezo yanayotolewa na wataalam kama vile Mukwa et.al. (2002) kwamba tathmini isitoe tu majibu kuhusu utendakazi wa wanafunzi bali kutathmini malengo ya masomo

yanayotolewa shuleni, mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, na mchakato mzima wa usomaji katika stadi hizi. Matokeo na mapendekezo kutokana na tafiti kama hizi huweza kuboresha tathmini tamati kwa kujumuisha matokeo ya tathmini endelevu.

v. Ikiwa lengo la kutathmini kusikiliza na kuzungumza ni kupima umilisi wa mwanafunzi katika stadi hizi, basi pana haja ya kuzitathmini kupitia njia ya usemi.

vi. Tathmini tamati katika kusikiliza na kuzungumza itolewe ifaavyo ili kutimiza sifa za tathmini bora za usahihi wa yaliyomo, kuaminika, matumizi ya matokeo yake, uhalali (kwamba inakinga dhidi ya udanganyifu), na uhalisia (Shiundu na Omulando, 1992).

vii. Kutumia njia mbadala ya imla kutathmini stadi hizi hata kama inachukuliwa na wengi kama ya kizamani mno na iliyopitwa na wakati.

viii. Baadhi ya shughuli za tathmini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza ni kama vile tathmini ya mahojiano ya moja kwa moja, maigizo, mazungumzo katika miktadha mbalimbali, mahojiano, utoaji wa hotuba, kushiriki katika mijadala, utoaji wa taarifa, matangazo kupitia vyombo vya habari, n.k. Shughuli hizi humsaidia mtahini kutathmini kujieleza kwa ufasaha, kuzingatia sarufi ya Kiswahili sanifu, kuzingatia matamshi sahihi huku akishirikisha matumizi ya kiimbo na shadda ili kuvipatia maana vipashio vya lugha na, matumizi ya msamiati kwa usahihi na panapofaa.

ix. Kushirikisha matokeo ya tathmini endelevu na tathmini tamati katika utuzaji wa vyeti, kuwaweka wanafunzi kulingana na viwango vya utendakazi, pamoja na kuwachuja ili kupata watakaoendelea na masomo ya viwango vya juu au kujiunga na vyuo anuwai. Hii ni kwa sababu kuna uwezekano mkubwa wa kutathmini stadi za kusikiliza na kuzungumza kupitia tathmini enedelevu.

x. Kuipa tathmini endelevu umuhimu zaidi kwa sababu inaonyesha maendeleo ya mwanafunzi katika kipindi kizima cha ujifunzaji na ufundishaji wa stadi ya kusikiliza na kuzungumza.

**Hitimisho**

Tathmini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza ina mchango mkubwa katika maisha ya mwanafunzi. Kwanza, hutoa majibu au itikio ambalo huarifu kuhusu maendeleo ya mwanafunzi katika kusikiliza na kuzungumza. Pia humweka mwanafunzi katika kiwango chake, ambacho hutumiwa kufanya uamuzi wa masomo atakayojiendeleza kwayo au kozi atakayochagua. Hivyo basi, ni jukumu la walimu na wanaotahini kuimarisha ufundishaji na ktathmini kupitia tathmini endelevu kutoa itikio na kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji, na kutumia matokeo ya tathmini tamati kwa lengo la kuwalinganisha wanafunzi. Aidha walimu na wanafunzi wanastahili kuweka msisitizo zaidi kwenye tathmini ya stadi za kusikiliza na kuzungumza na

kwamba kulingana na Butler & Stevens (1997), wanafunzi wanastahili kushiriki zaidi katika kukuza na kuendeleza stadi hizi mbili.

**Marejeleo**

Brown, H. D. & Abeywickrama, P. (2010). *Language Assessment: Principles and Language Practices*. Longman: Pearson Education

Frey, L., C. Botan, & Kreps, G. (1999). *Investigating communication: An introduction to Research Methods*. (2nd ed.) Boston: Allyn & Bacon.

Guyot, W. M. (1978). 'Summative and Formative Evaluation'. *The Journal of Business Education*. 54(3):127-129.

Hughes, A. (1989, 2003). *Testing for Language Teachers*. Cambridge: Cambridge University Press.

Kafwa, N. V. et al. (2014). 'The Revaluation Dilemma in Kenya Education System'. In *International J. Soc. Scie. And Education*. Vol. 4. Issue 2. pp

Kenya Institute of Education. (1992). *Primary Education Syllabus. Vol.1*. Nairobi: Kenya Institute of Education

Kenya Institute of Education. (1992). *Secondary Education Syllabus. Vol.1*. Nairobi: Kenya Institute of Education.

Kenya National Examinations Council. (2018). The Year 2017 KCSE Examination Report. Nairobi: KNEC.

Kenya National Examinations Council. (2018). The Year 2017 KCPE Examination Report. Nairobi: KNEC.

Lazaraton, A. and H. Riggenbach (1990). 'Oral Skills Testing: A Rhetorical Task Approach'. In *Issues in Applied Linguistics*. UCLA

Mukwa, C. and Too, J. K. (2002). General Instructional Methods. Eldoret: Moi University Press.

Murunga, F. (2016). 'Teaching of Listening Skills in Kiswahili Language: Instructional Strategies used by Secondary Teachers in Wareng Sub-county, Kenya. In *British Journal of Education*. Vol. 4. No 7. Pp 25-42.

Nasibi, W. 2003. Instructional Methods- Teaching Across the Curriculum. Nairobi: Strongwal Africa.

Piper, B. and Zuilkowski, S. S. (2015). 'Assesing Reading Fluency in Kenya: Oral or Silent Assessment?' In *International Review of Education*. Vol. 61. Issue 2. Pp 153-171.

Republic of Kenya. (1999). *Education for All, Issues and Strategies, 1991-2000 and Beyond*. Nairobi: Government Printers.

Rossett, A. K. S. (2001). *Beyond the Podium: Delivering Training and Performance to a Digital World*. San Francisco: Jossey-Bass/Pfeiffer

Shiundu, J. S. and Omulando, S. J. (1992). *Curriculum – Theory and Practice in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.